

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi saba (7) za kazi kwa ajili ya Ofisi ya Raisi Ikulu na nafasi mbili(2) za kazi kwa ajili ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kama ifuatavyo:-

### **OFISI YA RAIS IKULU**

#### **1. Afisa Takwimu Daraja la II (ZPSG - 08) nafasi 1 - Pemba**

##### **Sifa za waomabaji**

- i. Awe Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 46.
- ii. Awe amehitimu Shahada ya kwanza katika fani ya Takwimu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

#### **2. Fundi Umeme Daraja la III (ZPSD - 03) nafasi 1 Unguja na nafasi**

##### **1 Pemba**

##### **Sifa za waomabaji**

- i. Awe Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka arubaini na sita (46)
- ii. Awe amehitimu Stashahada ya ufundi umeme kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

#### **3. Fundi Vipaza Sauti (PA) Daraja la III (ZPSD - 03) nafasi 1 Pemba**

##### **Sifa za waomabaji**

- i. Awe Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka arubaini na sita (46).
- ii. Awe amehitimu “Full Technician Certificate (FTC)” au Stashahada ya “Telecommunication Engineering” au “Sound Engineering” kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

#### **4. Fundi Bomba Daraja la III (ZPSD - 03) nafasi 1 Pemba**

##### **Sifa za waomabaji**

- i. Awe Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka arubaini na sita (46)

- ii. Awe amehitim u kidato cha nne na amepata mafunzo ya ufundi bomba kwa ngazi ya cheti kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## **5. Fundi Simu Daraja la III (ZPSD - 03) nafasi 1 Unguja**

### **Sifa za waomabaji**

- i. Awe Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 46.
- ii. Awe amehitim Cheti cha Ufundi (VTA) au Cheti cha kawaida katika fani ya “Electrical Engineering” au “Telecommunication Engineering” au “Computer Engineering” au “Electronics Engineering” au “Mechanical Engineering” kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- iii. Awe na uzoefu na ujuzi wa kutengeneza simu.

## **6. Fundi Viyoyozi (AC) Daraja la III (ZPSD - 03) nafasi 1 Unguja**

### **Sifa za waomabaji**

- i. Awe Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 46.
- ii. Awe mwenye Cheti katika fani ya umeme au “Air Conditioning and Refrigeration” au nishati kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.

## **WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

### **1. Afisa Usafiri (TRANSPORT OFFICER) daraja la II (ZPSE -10) nafasi 1 Unguja**

### **Sifa za waombaji**

- i. Awe Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 46.
- ii. Mwenye Shahada ya kwanza ya usafirishaji (Logistic and Transport) au Usafiri Barabani (Road Transport) au Mhandisi Mitambo (Automobile Enginer) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

## **2. Afisa Uhusiano daraja la II (ZPSE -10) Nafasi 1 Unguja**

### **Sifa za waomabaji**

- i. Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka 46.
- ii. Awe amehitimu Shahada ya Kwanza katika fani ya Uhusiano wa Umma au Mawasiliano ya Umma kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### **Jinsi ya kuomba:**

- Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa maombi ya ajira (Zanajira) kupitia anuani ifuatayo:- <http://portal.zanajira.go.tz> kuanzia tarehe 14 April, 2023 hadi tarehe 29 April, 2023.
- Mfumo huo pia unapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini [www.zanajira.go.tz](http://www.zanajira.go.tz).
- Maombi yote yatumwe kwa anuani fuatayo:-  
KATIBU,  
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,  
S.L.P 1587,  
ZANZIBAR
- Muombaji anatakiwa kuanisha nafasi ya kazi aliyoomba.  
Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia email: [helpdesk@zanajira.go.tz](mailto:helpdesk@zanajira.go.tz) au simu Nam. 0773 101012.

**AHSANTENI.**